## “TEGA SIKIO UJIFUNZE” - KILA SIKU

# “Nini chanzo cha Mvua na Ngurumo za radi?”

**Mchezo umeandikwa na Leona Frommelt**

**Mwelekezi: Maja Dreyer**

**Wahusika:**

Jack Mvulana (14)
Jenny Msichana (14)
Metrolojia (Sauti kwa simu)

***Sehemu***
*Uwanja wa michezo*
*Nyumbani kwa Jack*

*Sauti*
Mtu akinywa maji
Glasi ikiwekwa mezani
watu wakicheza, Uwanja wa Michezo
maji ya kuchemka
Mfuniko wa Sufuria maji ya kichemka
Chai ikitiwa kikombeni
Mtu akikata simu
Ngumo za radi kutoka mbali kisha karibu
Mvua ikinyesha

**Utangulizi:(mtangazaji)**

Hujambo msikilizaji na karibu kwa mfululizo wa makala yetu ya tega sikio ujifunze.

Katika kipindi cha leo, Jenny na Jack wanatokwa na jasho, na sio eti tu ni kutokana na hali ya joto, bali maswali mengi ambayo hayajapata ufumbuzi.Wanafahamu fika kwamba afuani ya hali joto inayowakabili kwa sasa ni angalao manyunyu ya mvua.

Na miongoni mwa maswali hayo ,ni chanzo mvua. Licha ya Jack kujifanya hodari na mjuzi wa kila jambo, Jenny anafahamu vyema kuwa ni muoga wa ngurumo za radi.

**<u>SURA YA KWANZA</u>**

**Jenny na Jack wakutana katika uwanja wa michezo**

***(Mazingira; Sauti za chini kwa chini za watu wakicheza, wadudu, mpira,kipenga)***

Jack: Habari yako Jenny
*(Jack aendelea kubugia maji)*

Jack:. Jenny? kwani unataka kubugia lita ngapi za maji?

Jenny: *(Akiweka glasi mezani)* Nasikia vizuri sana. Hali yako Jack!

Jack : Sasa ukibugia maji namna hiyo, si utapasuka……?

Jenny: *(kicheko)* La hasha, nilikuwa na kiu cha kukata na shoka. Kwa kweli mimi siwezi kustahamili joto hili, na hasa ukiwa wewe ni mtu wa mazoezi, ni vyema unywe maji mengi tu… Hata wewe Jack, ingawa si mtu wa kupenda mazoezi, unapasa kunywa maji mengi tu!

Jack: Hata mimi angalau kupunguza hilo joto mwilini…
limezidi!… hasa katika muda wa wiki kadhaa za hivi punde.

Jenny: Kabisa,.Waonaje ikanyesha kidogo ..si itakuwa afueni?

Jack: Ha..ha.. waota wewe!.

Jenny: Nini chafanya ufikirie kutanyesha?

Jack: Mimi ni mwana Metrolojia chipukizi.

Jenny: Eti nani…….?

Jack: Mwana Metro..lo..ji..a chipukizi!

Jenny: Ebo..! Sio kukubeza lakini tangu lini?…. na hao Wanametrolojia kazi yao nini?.

Jack: *(kwa uangalifu)* Mwanametrolojia ni Mtabiri wa hali ya hewa. anaweza kutabiri mabadiliko ya hali ya anga!.

Jenny: Aala..!?. Hebu ni utahini utaalam wako. Kama unahakika hakutanyesha hivi karibuni ,basi nieleze chanzo cha Mvua.

Jack*: ( kwa jeuri)* kwani hujui? Unadhani kuna miungu Mvua, ambao huamua lini kunyeshe au kusinyeshe?

Jenny: Nieleze!

Jack: (kimya) Nitakueleza,, eehh….. kidogo tu nitakueleza kwa mtazamo wa kisayansi

Jenny: Sawa!, hata hivyo wacha nitatafuta ushauri wa mtaalam anieleze ni lini kutanyesha.

***Muziki….***

**SURA YA PILI *(NYUMBANI KWA JACK)***

Jenny: Nimeshukuru kwa mualiko wako wa kikombe cha chai.. Ehe!.. hebu nipashe kwa undani sababu ya yote haya?.

Jack: Wacha pupa,nilitaka tu kukupa mfano wa chanzo cha mvua kwa kutumia,haya maji moto. Na kisha baadaye tuandae kikombe cha chai... je upo? *(sauti ya maji ya kichemka)*

Jenny: Nipo!

Jack: Cha msingi ni uelewe kwamba maji yaliyo mfumo wa Mvuke ambao hufuka wakati wote kati ya mbinu na ardhi, na kisha mvuke huo unapo poa, hubadilika na kuanza kunyesha mvua.

Jenny: Nimeshika sikio!, lakini hilo lahusiana vipi na mfano huu wa sufuria ya maji moto?.

Jack: Hebu tizama kwa makini, ninapo funika sufuria hii,*(sauti ya mfuniko ukigongana na sufuria)*, na kisha unapo ufunua baada ya muda maji yakichemka, mvuke hukusanyika kwenye sufuria. Hii ni kwasababu moto huyabadilisha maji kwenye sufuria na mfumo wa mvuke…. tuko pamoja?

Jenny: Kisha ….?

Jack: Unamana mvuke umekusanyika katika mfuniko huu na kuwa matone ya maji, kisha kuanza kudondoka taratibu kwenye sufuria. Kwa hivyo huu ni mfano wa mvua ikinyesha ndani ya sufuria?

Jenny: Hapo nimekuelewa … .. mfano huu wa sufuria, moto na mvuke!. Kwa hivyo unamaanisha huu mfuniko ni mfano wa mbingu?.

Jack: Hasa!,…. Kumbuka kwamba asilimia 70 ya ardhi imefunikwa na maji, na kutokana na miale ya jua, maji huwa moto.Katika mfano huu wetu, tumeona jinsi jiko linavyo chemsha maji haya kutoka chini, lakini miale ya jua huyafanya maji yaliyoko ardhini kupata, na kisha yanapokuwa moto yakabadilika na kuwa mvuke. Mvuke huu kisha hufuka hadi mbinguni. Kadri mvuke huu unavyozidi kufuka juu ndivyo unavyokuwa baridi, kwani sharti uelewe kwamba unavyozidi kupanda ndivyo hali ya baridi inavyozidi.

Jenny: Sasa nimekuelewa….ehh, Unamaanisha hewa baridi angani ni mfano wa mfuniko huu ambapo Mvuke unaposhika baridi hunageuka na kuwa matone ya maji.

Jack: Hasa!….. lakini kabla hayo mvuke huu hukusanyika na kuwa mawingu. Mawingu yanauwezo wa kufuka umbali wa mita 5,000 angani ambako huwa na baridi ya nyuzi 20 chini ya sufuri. Na unaelewa kwamba maji huwa theluji chini ya nyuzi Sufuri.Kwa hivyo Mvuke huu hushikana na kuwa madonge ya maji, na kadri yanavyoendelea kushikana ndivyo yanavyokuwa mazito na hapo mvua huanza kunyesha.

Jenny*: (akiwa amechanganyikiwa)* Sasa madonge haya hayawezi kumumiza Mtu?.

Jack: La hasha!..ukumbuke wakati madonge haya yanapodondoka ardhini, hupitia tandu za hewa moto na hivyo basi kuyeyusha madonge haya na hatimaye kunyesha mvua ardhini.

Jenny: Naomba tu kunyeshe hivi sasa kwani joto hili litatuyeyusha!.

Jack: Je, ulifanikiwa kumpata Metrolojia?

Jenny: Ndio, nilipiga simu na kuzungumza na mmoja wao ofisini.

Jack: Na Je, alikueleza nini chanzo cha Mvua? .

Jenny: Naam, lakini siwezi kukuambia, kwanza nipate kikombe cha chai ulichoniahidi!

Jack: Oh, pole!,.. Karibu nisahau…. *(Jack amtilia chai Jenny)*

***Muziki…***

SURA YA TATU *(Bado ni nyumbani kwa Jack*)

Jack: Sasa niambie, ni yapi aliyokukwambia mtabiri huyo wa hali ya anga?.

Jenny: Alitabiri mvua ya ngurumo za radi itanyesha hivi leo!..

Jack: Hewala, bila shaka hizo ni habari njema, angalau kiwango cha joto kipungue kidogo, japo nadhani mvua hiyo ya ngurumo za radi haitadumu.

Jenny: Ala..!, kwani metrolojia huyu chipukizi ni muoga wa Ngurumo za radi?

Jack: Wala sitakuficha!, hali yangu taabani hasa inapoyesha ya ngurumo za radi…..

Jenny: Nani ataamini Jack na ujasiri wake ni muoga wa Ngurumo za radi!.

Jack: Wacha kejeli zako Bw..! Kwani huyo mwanametrolojia hawakueleza athari ya ngurumo za radi?.

Jenny: Aliniambia,… na zaidi akanielimisha kuhusu chanzo cha ngurumo za radi!.

*muziki wa chini kwa chini kisha mazungumzo*

Metrolojia *(Sauti ya Mtu akiongea kwa simu)* Ni jambo la kushangaza sana Jenny. Wakati wa ngurumo za radi, upepo mkali huyatenganisha madonge mepesi na yale mazito kwenye wingu.Kisha madonge mepesi husukumwa juu ya wingu ilhali yale mazito kuja chini ya wingu hilo. Hali hiyo huongezeka baina ya mawingu na pia kati ya mawingu na Ardhi. Na mwishowe mukurumbiano huo ukatoa cheche kuashiria ngurumo za radi.

Jenny: Na ni lazima ujihadhari wakati wa ngurumo za radi.

Meteorolojia: Bila shaka, kwani muale wa Radi huwa na kiwango cha joto hadi nyuzi 30,000.

Jenny: Na Je ngurumo?.

Metrolojia: Kwa kuwa Radi huwa na moto mkali, hewa iliyoko karibu na miale hiyo ya radi hupata moto kwa haraka na kusababisha sauti kama mlipuko. Kasi ya miale ya radi ndiyo husababisha ngurumo.

Jenny: Na kwanini radi huonekana kabla ya Ngurumo?

Metrolojia: Radi ina kasi ya mwanga kuliko sauti. Lakini huwezi kuona haya iwapo huko katika eneo la matukio.

Jenny: Na hilo ndilo linalomtia hofu zaidi Jack!

Metrolorologiji: Jack ni Nani?

Jenny: Ni rafiki yangu.Lakini ni muaga sana wa ngurumo za radi. Hata hivyo nimeshukuru sana kwa maelezo yako

Meteorologist: Karibu tena! ukiwa na swali usisite kunipigia simu wakati wowote.kwaheri *(akikata simu)*

*muziki ukitoweka pole pole:*

Jack: Kwa kweli mimi sitishiki na Ngurumo za radii ila tu zanitia hofu.

Jenny:Jack, Unajua kwamba umebahatika kuwa na rafiki kama mimi? najua sasa nitafanya nini wakati wa mvua ya ngurumo za radi.

Jack: Nini?

Jenny: Nitakueleza punde tu itakapoanza kunyesha

*Muziki*

SURA YA NNE: Bado Nyumbani kwa Jack:

*( Sauti ya ngurumo za radi kwa mbali kisha zikikaribia).*

Jack: Jenny,Naona mvua karibu kunyesha sasa.

Jenny:Lakini hatuna wasi wasi tuko nyumbani hapa.

Jack: Je, ingelikuwaje kama hii mvua ingetupata nje kwa ghafla?.

Jenny: Tungejingika kwanza, mfano ndani ya gari. Ukjiwa ndani ya gari uko salama, unajua vyuma husaidia au hukukinga dhidi ya miale ya radi na kuelekeza ardhini.Pia unapasa kuepuka vilele, kwani radi huwa na madhara makubwa unapokuwa kileleni. Kwa mfano juu ya Mti, mlingoti au ua za stima.

Jack: Na Je, iwapo uko mahala wazi pasipo na kinga?

Jenny: Unaweza tu uchuchumae huku sehemu ya mwili iikiwa imegusa ardhi na mikono yako kati kati ya miguu.Zaidi usithubutu kuwa ndani ya maji au kuogelea wakati wa radi

Jack: Kwasababu maji ni kiungo muhimu cha kupitisha nguvu za umeme.

Jenny: Naam.

*(sauti ya Ngurumo za radi yaongezeka)*

Jack: Asante sana najua nikiwa na wewe sina wasi wasi wowote wa kuogopa radi.

Jenny: Hayo ndio manufaa ya kuwa na rafiki wa dhati. Tufurahie Mvua Bwana!.

*(mvua ikinyesha)*

Jack: Kweli, tunapasa kufurahia mvua Jenny!.

*Muziki…….. Mwisho*

(Mtangazaji)

Bila shaka mvua hiyo itakuwa afueni kwa marafiki hawa wawili. Lakini kama tutakavyosikia hivi punde, bado marafiki hawa wa dhati Jack na Jenny, wanakabiliwa na mitihani mkubwa usoni. Ni hayo tu kwa leo mpenzi msikilizaji wa kipindi cha tega sikio ujifunje, lakini unaweza pia kutusikiliza kupitia mtandao wetu www.dw.de/kiswahili. Mchezo huu umeandikwa na Leona Fromelt . Hadi wakati mwengine ---Kwaheri.